

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mkuu wa TAKUKURU (M) Kinondoni,
S.L.P 90397, Kinondoni
Simu : 222170852 Nukushi 2170963
Barua pepe: rbckinondoni@pccb.go.tz
Wavuti www.pccb.go.tz

WAFIKISHWA MAHAKAMANI KWA KOSA LA WIZI, KUGUSHI NA KUISABABISHIA SERIKALI HASARA YA TSH 569,325,000/=

Aliyekuwa Mhasibu Mwandamizi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) Bw. Isaya Paul Philip (39) mkazi wa Kimara Dar es Salaam na watumishi 11 wa Benki ya CRDB, Tehan Bino Spendy; Jones Joseph Lisso; Adelphina Modest Barongo; Daniel Kahamba; Benedicta Zelamula Boniface; Edna Rwiza; Ally Mohamed Hamad; Msafiri Abdallah Sobu; Anthony Festo Moshi,; Aisha Ismail Mussa na Khaji Selemani leo wamefikishwa Mahakamani mbele ya Mh. F. Moshy kwa makosa 404 ikiwa ni pamoja na kosa la kuisababishia Serikali hasara ya jumla ya Tsh 569,325,000/= (Milioni Mia Tano Sitini na Tisa, Laki Tatu na Ishirini na Tano Elfu), fedha za Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

Washitakiwa wote wamefikishwa Mahakamani na TAKUKURU (M) Kinondoni leo tarehe 08/10/2018 kujibu mashitaka yanayowakabili chini ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007, Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 kama ilivyorekebisha Mwaka 2002 pamoja na Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 kama ilivyorekebisha Mwaka 2002. Washitakiwa wote wanadaiwa kutenda makosa hayo kati ya Mwaka 2010 na 2013.

Mkuu wa TAKUKURU (M) wa Kinondoni Bi. TERESIA MNJAGIRA anawaasa Watumishi wa Umma, Watumishi wote wa Serikali pamoja na Taasisi binafsi hasa za kifedha kuheshimu nyadhifa zao na kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria bila kujihusisha na vitendo vya Rushwa au vitendo vingine vya kijinai. Pia, anatoa wito kwa Wananchi wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU kwa kuwafichua wale wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa ili waweze kuchukuliwa hatua za kisheria kwani kwa kufanya hivyo tutakuwa tumezia vitendo hivyo visiendeleo kujitokeza katika Jamii yetu.

**IMETOLEWA NA KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M) KINONDONI
EUGENIUS HAZINAMWISHO**

08/10/2018
